CRDB BANK

*Tunakusikiliza*

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 28

Mwenyekiti na Wanahisa,

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nane wa CRDB Bank Plc utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 20 Mei 2023, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba na kwa njia ya kidijitali kuanzia saa tatu kamili (Saa 3.00) asubuhi kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba uliopita.**
4. **Kujadili yatokanayo na kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba**
5. **Kujadili na kupokea Ripoti ya Wakurugenzi wenye dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2022.**
   5.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.
   5.2 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2022.
   5.3 Gawio kwa mwaka 2022.
6. **Kuidhinisha ada ya Wakurugenzi.**
7. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.**
8. **Kuchagua Wajumbe wawili Huru wa Bodi**
9. **Kujadili mapendekezo kutoka kwa Wanahisa.**
10. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
11. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao.**
12. **Kufunga Mkutano.**

***MAELEZO:***

*1. Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 11/05/2023 na litafunguliwa tena tarehe 12/05/2023.*

*2. Mapendekezo kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 9 yatumwe na yamfikie Katibu kabla ya Alhamisi tarehe 27/04/2023 saa 10.00 jioni.*

*3. Makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana matawini na yanaweza kuchukuliwa kuanzia tarehe 10/05/2023, vinginevyo yatapatikana Arusha kwenye ukumbi wa mkutano tarehe 19 hadi 20 Mei 2023. Pia makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana kwenye tovuti ya benki www.crdbbank.co.tz kuanzia tarehe 10/05/2023*

*4. Wanahisa wanaotaka kuhudhuria Mkutano Mkuu watajigharamia usafiri na malazi.*

**TAARIFA YA SEMINA KWA WANAHISA**

Taarifa inatolewa kwamba kutakuwa na Semina kwa Wanahisa itakayolenga kutoa elimu kuhusu Uwezeshaji kwa Vijana na Wanawake Uanzishwaji wa Vyeti Elektroniki vya Umiliki wa Hisa, Upigaji wa kura kwa mfumo wa kidijitali na Ushiriki wa Benki ya CRDB katika mageuzi ya kiuchumi nchini Tanzania itayofanyika Ijumaa, tarehe 19/05/2023 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba kuanzia saa 3.00 asubuhi Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatavyo:

Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatavyo:

**Katibu**
**CRDB Bank Plc**
**S. L. P. 268**
**Dar-es-Salaam**
**Barua pepe -shares_unit@crdbbank.co.tz**
**Namba ya kiganjani 0755 197 700**
**Namba ya WhatsApp 0767 757 215**

KWA IDHINI YA BODI

J. B. Rugambo
**KATIBU**

19 Aprili, 2023